


HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA
(Barua zote ziandikwe kwa mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya)

Simu: 028 2590162
Nukushi: 028 2590249



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 44
BUCHOSA-SENGEREMA

Kumb.Na.AB.74/211/01/6

15/05/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kuweza kuajiriwa katika kazi zifuatazo

1. Muuguzi daraja la II –7

- a) **Sifa za kuajiriwa:Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-**
- Elimu ya kidato cha nne au sita
 - Awe na Cheti cha Uuguzi cha miaka isiyopungua mitatu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania Mwaombaji awe na uzoefu wa usiopungua miaka mitatua.

b) **Kazi za kufanya**

- Kusimamia na kuratibu kazi zote za uuguzi katika sehemu ya kazi
- Kutoa ushauri nasaha kwa wateja/Wagonjwa
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

- c) **Mshahara:** Mtumishi atakayefanikiwa kuajiriwa katika nafasi hizi, atalipwa mshahara utakaoanza ngazi ya TGHS A

2. Mtekinolojia Daraja II-7

- a) **Sifa za kuajiriwa:Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-**
- Elimu ya kidato cha nne au sita

- ii. Awe na Stashahada katika fani ya Utekinolojia ya muda wa miaka mitatu katika moja ya maabara.

b) Kazi za kufanya

- i. Kupima sampuli zinazoletwa maabara
- ii. Kuhifadhi Sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu
- iii. Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, Vitendanishi, Vifaa, Kemikali na hifadhi ya kemikali
- iv. Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi
- v. Kufundisha watumishi walio chini yake
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

- c) **Mshahara:** Mtumishi atakayefanikiwa kuajiriwa katika nafasi hizi, atalipwa mshahara utakaoanzia ngazi ya TGHS B

3. Tabibu II-3

a) Sifa za kuajiriwa:Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- i. Elimu ya kidato cha nne au sita
- ii. Awe na Stashahada ya Utabibu ya muda wa miaka mitatu katika chuo kinachotambuliwa na serikali

b) Kazi za kufanya

- i. Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
- ii. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo
- iii. Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za afya Msingi
- iv. Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za afya za mfuko wa Afya ya Jamii
- v. Kuweka Kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
- vi. Kuweka Kumbukumbu, Kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji

- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake
- c) **Mshahara:** Mtumishi atakayefanikiwa kuajiriwa katika nafasi hizi, atalipwa mshahara utakaoanzia ngazi ya TGHS B

Masharti ya Kazi zinazotangazwa

- i. Ajira hizi zitakuwa za mikataba wa mwaka mmoja mmoja kwa kuzingatia kipindi chote ambacho wafadhili watagharamia ajira zao.
- ii. Kipindi cha ufadhilli kikimalizika, watumishi hawa hawataingizwa moja kwa moja katika utaratibu wa Ajira za serikali bali itategemea ufanisi na utendaji kazi wao
- iii. Ajira hizi zinaweza kuendelea baada ya mikataba yao kuisha kwa masharti ya Mikataba kwa mishahara inayotokana na malipo ya makusanyo ya ndani ya vituo husika au kutoka katika halmashauri husika.

Mambo ya Muhimu ya kuzingatia

1. Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania
2. Awe na Umri kuanzia miaka 18 hadi 45
3. Awe mwadilifu asiwe na historia ya uhalifu

Wananchi wenye sifa wanatakiwa kutuma maombi yao yakiambatana na vivuli/nakala za vyeti vyta elimu na taaluma pamoja na vyeti vya kuzaliwa kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa
S.L.P.44 Buchosa- Sengerema

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/05/2018 saa tisa kamili alasiri.


MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BUCHOSA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA